# ANDIKO LA KISERA

JULAI 2020

13 HATUA DHIDI YA MABADILIKO YA TABIANCHI

15 UHAI KATIKA ARDHI



## USIMAMIZI WA MAENEO YA MALISHO

## WITO WA KUWA NA MTIZAMO MPANA

Andiko hili la kisera linatokana na uzoefu uliopatikana katika utekelezaji wa miradi mitano ya ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi nchini Tanzania, iliyofadhiliwa na Umoja wa Ulaya chini ya Mpango wa Global Climate Change Alliance (GCCA) na kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2015 mpaka 2019. Miradi ya GCCA ipo katika kanda tofautitofauti za ikolojia-kilimo (agro-ecological zones). Andiko hili la kisera linaelezea kwa ufupi mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza katika kuboresha usimamizi wa maeneo ya malisho katika maeneo ya wafugaji. Andiko linatoa ujumbe muhimu na mapendekezo ya kisera yatakayosaidia katika usimamizi endelevu wa maeneo haya ya malisho.

**Miradi mitano ya GCCA nchini Tanzania:**

- **Misitu ya Jamii Pemba** – Ukuzaji wa Ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi: (Community Forests Pemba – scalable Resilience: Outspreading Islands of Adaptation)
- **EcoACT** – Njia za kiikolojia za Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Katikati mwa Tanzania (Dodoma) (Eco-Village Adaptation to climate change in Central Tanzania), Dodoma
- **ECOBOMA** - Mfano wa Ustahimilivu wa tabianchi kwa jamii za wafugaji za mbuga za Maasai (A climate Resilient Model for Maasai Steppe Pastoralists), Arusha
- **Mradi wa Eco-village Igunga** (Igunga Eco-village project)
- Mbinu Jumuishi za Kustahimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Milima ya Usambara Mashariki (Integrated Approaches for Climate Change Adaptation in the East Usambara Mountains), Muheza

GCCA+
THE GLOBAL CLIMATE CHANGE ALLIANCE PLUS INITIATIVE
Kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya
TANZANIA

## UJUMBE MUHIMU

- Tanzania haina sera ya kitaifa ya maeneo ya malisho inayozingatia mahitaji maalumu ya wafugaji wa kuhamahama.
- Jamii za wafugaji wa kuhamahama zina sifa kuu za uchungaji wa mifugo kwa mzunguko na uhamaji wa maeneo na sifa hizi zinaongezeka zaidi kutokana na ongezeko la ukame unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi
- Uwepo wa uwiano wa upatikanaji wa maji na malisho ni jambo muhimu katika maeneo ya malisho ili kuepusha uchungaji wa mifugo unaozidi uwezo wa eneo.
- Ukosekanaji wa mwongozo wa kisheria unaotambua maeneo ya malisho na shoroba za wafugaji wa kuhamahama huchochea migogoro dhidi ya matumizi mengineyo ya ardhi.
- Taratibu zilizozoeleka za upangaji wa matumizi ya ardhi hujikita katika ngazi ya Kijiji na haziangalii hali fulani zilizo maalumu katika maeneo ya malisho, kama vile mahitaji ya kuhamahama katika eneo kubwa.
- Ni muhimu kuwa na ushirikishwaji thabiti wa jamii za wafugaji, wakiwamo viongozi wa kimila katika usimamizi shirikishi wa maeneo ya malisho na maji ili kuhakikisha uendelevu na kupunguza migogoro.
- Kwa ujumla, usimamizi wa sheria ndogondogo zinazohusu usimamizi wa maeneo ya malisho ni duni kutokana na uwezo mdogo wa mamlaka za wilaya na vijiji, na hivyo kuhitaji njia mbadala.
- Kuna ukosefu wa taarifa kuhusu hali ya maeneo ya malisho. Ukosefu huu unaweza kutatuliwa kupitia njia shirikishi za ufuatiliaji zinazohusisha wanajamii hasa vijana.

## MAPENDEKEZO MUHIMU

- Sera za maeneo ya malisho zinahamasisha uanzilishwaji wa misitu ya jamii itakayoweza kusaidia kuwa kimbilio kipindi cha ukame, na upandaji wa miti katika maboma ili kupunguza ukataji miti ovyo.
- Upangaji katika ngazi ya uwanda mpana unapaswa kuhamasishwa katika maeneo ambayo rasilimali, kama vile maeneo ya malisho katika vijiji, yanatumiwa kwa ushirikiano.
- Ushirikishwaji wa mamlaka za vijiji, vikundi vya wafugaji na viongozi wa kimila katika programu za usimamizi wa maeneo ya malisho unapaswa kuhimizwa ili kuongeza uendelevu wa mfumo wa ikolojia ya maeneo ya malisho.
- Miongozo wa miundombinu ya maji katika maeneo ya malisho inapaswa kuweka kipaumbele katika umuhimu wa uwiano katika upatikanaji wa maji na malisho na katika mchakato shirikishi na kujengea uwezo kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi makini wa miundombinu.
- Kuwezesha ardhi ya kimila ya ufugaji, shoroba za wafugaji na njia kuu za wafugaji kuwa na nguvu ya kisheria
- Mbinu shirikishi zaidi za usimamizi wa utekelezaji wa sheria ndogondogo za maeneo ya malisho zinapaswa kujumuishwa katika sera na programu, kwa mfano, kwa kuwashirikisha vijana kama askari jamii.
- Matumizi ya mfumo wa usimamizi shirikishi katika jamii kubwa za wafugaji unapaswa kuhamasishwa ili kuongeza taarifa za hali ya maeneo ya malisho na kuboresha michakato ya upangaji.

## UTANGULIZI

Tanzania haina sera maalumu ya ufugaji katika ngazi ya taifa inayozingatia mahitaji ya wafugaji wanaohamahama. Sera ya Taifa ya Mifugo (2006) inalenga kuboresha usimamizi na matumizi ya maeneo ya malisho ili kusaidia uzalishaji endelevu wa mifugo na uboreshaji maisha ya wafugaji. Hata hivyo, sera haina maelekezo ya wazi kuhusu usimamizi shirikishi wa maeneo ya malisho, ufuatiliaji madhubuti wa kiikolojia na huduma za ushauri kwa wafugaji na wala sera haielezi kwa umahususi ni kwa vipi miundombinu ya maji itajumuishwa katika usimamizi wa maeneo ya malisho katika maeneo ya wafugaji.

Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya 2007 inaelekeza Halimashauri za Wilaya zikiwa kama Mamlaka za Upangaji za Wilaya kushirikiana na wadau wengine kuandaa mipango ya wilaya ya matumizi ya ardhi na kuratibu shughuli za upangaji matumizi ya ardhi za vijiji. Hatua za kawaida za upangaji ardhi zimejikita katika ngazi za vijiji na hazihusishi hali mahususi katika maeneo ya malisho, hasa mahitaji ya kuhamahama katika uwanda mpana kwa jamii za wafugaji wanaohamahama.

Maisha ya wafugaji katika ardhi kame kama vile Mbuga ya Maasai, hutegemea moja kwa moja upatikanaji wa huduma za kiikolojia. Katika Mbuga ya Maasai, kuna uthibitisho wa wazi kwamba mabadiliko ya tabianchi tayari yameathiri mfumo wa ikolojia kwa kiasi kikubwa. Kwa kadiri ambavyo rasilimali ya maji inaendelea kuwa adimu, mifugo nayo hulundikana sehemu moja na kusababisha uchungaji wa kupita uwezo wa eneo na uharibifu wa ardhi.

Katika programu ya GCCA Tanzania, hususani katika mradi wa ECOBOMA uliofanyika Arusha uliojishughulisha na kujenga uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wafugaji wa Kimaasai walio hatarini. Changamoto na mapendekezo yaliyoorodheshwa hapa chini yametokana moja kwa moja na uzoefu wao na mambo waliyojifunza.

## CHANGAMOTO

### Athari za matukio ya hali ya hewa yasiyo ya kawaida

Vipindi virefu vya ukame vya mwaka 2016 na 2017 katika eneo la mradi wa ECOBOMA (katika wilaya za Meru na Arusha) vilisababisha janga kubwa la kupungua kwa malisho na uhamaji mkubwa wa mifugo nje ya eneo la mradi. Ukame mkali na wa muda mrefu pia ulisababisha baadhi ya wafaidikia kujazilizia kipato chao kwa kujihusisha na shughuli zisizo endelevu kama vile uzalishaji wa mkaa na ukataji kuni kwa ajili ya kuuza.

Tofauti na ukame, matukio ya mvua nyingi kupita kiasi ya mwaka 2018 yalisababisha mafuriko na uharibifu wa miundombinu ya maji iliyokarabatiwa na mradi wa ECOBOMA, kudhihirisha kwamba athari za mabadiliko ya tabia nchi ni za namna nyingi.

### Kuhusisha viongozi wa kimila katika shughuli za maendeleo

Viongozi wa kimila wa jamii ya Wamasai wana nafasi kubwa sana katika jamii. Katika hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa ECOBOMA ilikuwa ni changamoto sana kuwashirikisha viongozi hawa (wanaume na wanawake) kwa sababu timu iliyohusika na mradi haikuwa na hadhi ya kimila ya kuchangamana na viongozi hawa. Masuala haya ya kitamanduni yalisababisha wanawake kutokujitokeza katika baadhi ya shughuli za mradi, kama vile kujihusisha katika kamati za usimamizi wa malambo.

Kwa kupitia wazee na wapatanishi wa kijamii wanaoheshimika sana katika jamii, mradi wa ECOBOMA ulifanikiwa kutanzua changamoto hii na kuboresha mawasiliano kati ya viongozi wa kimila na mamlaka za serikali za mitaa. Wapatanishi hawa walikubali mijadala, walijibu maswali kwa ufasaha na walifanya upatanisho pale walipohitajika, ili kupunguza migogoro mingoni mwa jamii lengwa.

### Kukosekana kwa mipango ya ardhi katika ngazi ngazi ya uwanda mpana kwa ajili ya wafugaji

Sheria ya Matumizi ya Ardhi ya mwaka 2007 inalenga kuboresha upatikananaji na udhibiti wa rasilimali wa wanajamii. Sheria inaeleza taratibu za mchakato

wa upangaji vijiji kwa kuanzisha Mamlaka ya Upangaji Vijiji, ambayo ni Halimashauri ya Kijiji na taratibu za kuandaa mipango ya vijiji. Hata hivyo, katika maeneo ya wafugaji, upangaji katika ngazi ya kijiji hauzingatii mazingira ya uwanda mpana ambayo wafugaji wanayatumia katika uchungaji wa mifugo yao. Kunahitajika upangaji katika ngazi ya uwanda mpana, na tafsiri ya uwanda kwa ujumla ikiwa ni rasilimali za maeneo ya malisho ambazo wafugaji hupita mara kwa mara katika mwaka mzima wakitafuta malisho na maji.

### Usimamizi mdogo wa sheria ndogondogo za maeneo ya malisho

Maeneo ya malisho yameendelea kukabiliwa na ukataji miti na uchungaji wa mifugo kinyume cha taratibu zilizowekwa kutokana na usimamizi duni wa sheria ndogondogo. Mamlaka za wilaya na vijiji vinapaswa kushinikiza usimamizi wa sheria ndogondogo ili kulinda maeneo ya malisho hatahivyo zinakabiliwa na uhaba wa rasilimali (watu na fedha). Mradi wa ECOBOMA kwa kushikiana na Mamlaka za Wilaya, ulitatua changamoto hii kwa kutoa mafunzo ya uaskari jamii kwa vijana wa vijijini. Askari Jamii hao walipewa mamlaka ya kuhakikisha uzingatiwaji wa sheria ndogondogo zilizopitishwa kama vile za kuzuia uzalishaji mkaa.

### Kukosekana kwa uratibu makini na miongozo ya usimamizi wa rasilimali katika jamii za wafugaji

Uratibu kati ya wadau kutoka sekta za Mifugo, Kilimo, Misitu, Maji, Ardhi na Wanyamapori ni mdogo, jambo ambalo lina athari hasi katika uendelevu wa utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maeneo ya malisho, ikiwemo usanifu na usimamizi wa miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo.

Mradi wa ECOBOMA ulijifunza kwamba mafanikio ya miundombinu ya maji kwa ajili ya mifugo kama vile malambo yalitegemea kwa kiasi na maarifa mazuri ya kiufundi lakini kwa sehemu kubwa yalichangiwa na usimamizi mzuri na imara wa wanajamii. Hata hivyo, miongozo ya serikali kwa kiasi kikubwa imejikita katika usanifu wa kiufundi na hauzingatii upande wa usimamizi.

### Kukosekana kwa taarifa za hali ya maeneo ya malisho

Taarifa nzuri na zinazoendana na wakati kuhusu hali ya maeneo ya malisho zinatakiwa ili kuhakikisha upangaji na matumizi makini ya rasilimali za malisho kwa ajili ya mfumo wa maisha ya wafugaji. Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania taarifa hizo hazipatikani.

Mradi wa ECOBOMA imeshughulikia changamaoto hii kwa kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji ambao umeundwa ili utumike na kutekelezwa na jamii za wafugaji zenyewe, kuwawezesha kufanya uamuzi sahihi yanayotokana na taarifa, kuhusu usimamizi wa maeneo ya malisho. Taarifa hizo za ufuatiliaji zinaweza pia kutumika kama nyenzo ya upangaji wa ngazi ya uwanda mpana katika maeneo yenye maeneo makubwa ya malisho.

## MAPENDEKEZO YA KISERA

### Kuanzisha misitu ya jamii na kuizungushia uzio

Kutokana na kuongezeka kwa hali ya ukame inayotokana na mabadiliko ya tabianchi, ni muhimu kutenga maeneo maalumu katika maeneo ya malisho ambayo yatakuwa ni kimbilio, ambapo uchungaji wa mifugo utaruhusiwa tu katika kipindi cha ukame uliokithiri. Maeneo hayo yanaweza kutengwa kama Misitu ya Jamii katika ardhi za Vijiji yenye sheria ndogondogo zinazoeleza vigezo vya matumizi na uhifadhi.

Changamoto katika rasilimali za misitu zinaweza kupunguzwa kwa kuanzisha upandaji miti inayofahamiaka kwa kimaasai kama 'Osilalei' (commiphora) na minyara (minyaa) kama fensi ya kudumu ya maboma badala ya kujenga kwa kutumia matawi ya miti ambayo huhitaji kubadilishwa mara kwa mara.

### Hakikisha ushiriki wa viongozi wa kimila katika usimamizi wa maeneo ya malisho

Uzoefu uliopatikana katika mradi wa ECOBOMA unaonesha kwamba ushirikishwaji wa viongozi wa kimila katika michakato yote ni muhimu ili kuhakikisha uendelevu wa mradi. Pia husaidia kupunguza migogoro ya matumizi ya maliasili hasa katika msimu wa ukame na kuongeza kiwango cha uaminifu na ushirikiano kati ya viongozi wa kimila na serikali za mitaa.

Mojawapo ya mafanikio makubwa ya mradi wa ECOBOMA katika suala hili ni uwepo wa ushirikiano wa karibu ulioanzishwa kati ya Askari Jamii na Maofisa Wanyamapori wa Wilaya.

### Hamasisha upangaji wa pamoja wa ardhi katika ngazi pana ya uwanda

Katika maeneo ya Kaskazini mwa Tanzania rasilimali za malisho hutumiwa na jamii nyingi, hivyo zinahitaji mpango wa matumizi ya ardhi na rasilimali katika ngazi ya uwanda mpana kuliko ngazi za vijiji. Tume ya Taifa ya Upangaji Matumizi ya Ardhi inasaidia wadau katika kuanzisha Upangaji huu wa pamoja wa Matumizi ya Ardhi na kutoa cheti cha kimila cha haki ya umiliki kwa jamii. Sera za Taifa za Mifugo na Ardhi zinapaswa kutambua upangaji wa aina hii na hasa upangaji wa pamoja wa ardhi za vijiji katika maeneo ambayo rasilimali kama vile maeneo ya malisho hupatikana katika pande zote za mipaka ya vijiji vinavyopakana.

### Wezesha usimamizi wa sheria ndogondogo za maeneo ya malisho

Mamlaka za wilaya na vijiji hazina rasilimali za kutosha kuhakikisha usimamizi kamilifu wa sheria ndogondogo zinazosaidia uwepo wa matumizi endelevu ya maeneo ya



malisho. Mradi wa ECOBOMA ulishughulikia tatizo hili kwa kufanya kazi kwa pamoja na mamlaka za wilaya ili kusaidia kuanzisha na kutoa mafunzo kwa timu ya Askari Jamii wakiwa ni vijana wa vijiji husika. Mbinu hizo shirikishi za usimamizi madhubuti wa sheria ndogondogo zinapaswa kuwezeshwa kupitia sera za taifa na programu za maendeleo.

### Kuboresha uratibu na miongozo ya usimamizi wa maji ya mifugo katika maeneo ya malisho

Usimamizi wa rasilimali za maji na malisho unapaswa kuratibiwa na kujumuishwa katika ngazi ya jamii na ngazi ya uwanda mpana wa maeneo ya malisho. Kwa kuboresha ushirikiano kati ya wadau wote katika maeneo ya wafugaji, kuna nafasi ya kuboresha usimamizi wa maji katika maeneo ya malisho, na kwa ujumla kuchangia moja kwa moja katika ustawi wa ikolojia ya maeneo ya malisho.

Miongozo ya miundombinu ya maji ya mifugo kwa ajili ya maeneo ya malisho inatakiwa izingatie vyema uwiano wa upatikanaji wa maji na malisho na kusisitiza umuhimu wa michakato shirikishi na kujengea uwezo kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi makini wa jamii wa miundombinu, kwa mfano, kupitia kamati ya malambo kama ilivyofanyika katika mradi wa ECOBOMA. Miongozo ya kitaalamu ya ujenzi wa malambo unapaswa pia izingatie uwezekano wa kuongezeka kwa mvua na mafuriko kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

### Hamasisha usimamizi shirikishi wa kiikolojia

Ukosefu wa taarifa za hali ya maeneo ya malisho huzuia upangaji wenye ufanisi kwa ajili ya usimamizi endelevu wa maeneo ya malisho. Mfumo wa ufuatiliaji shirikishi unaojumuisha wanajamii na mamlaka za kijamii unaweza kufaa katika ufuatiliaji wa hali ya maeneo ya malisho, na katika kupendekeza njia za kijamii za kushughulikia changamoto zilizobainika. Mfumo ulioanzishwa na kutekelezwa na mradi wa ECOBOMA unaweza kutumika kama modeli ya mfano katika kuboresha usimamizi wa kiikolojia wa maeneo ya malisho nchini Tanzania, na kuleta uelewa mzuri wa hali ya maeneo ya malisho na changamoto zake zinazohitaji ufumbuzi.

### Marejeleo


GCCA Tanzania, (2018). Annual reports and case studies

Sendalo, D.S. (2009). A Review of Land Tenure Policy Implications on Pastoralism in Tanzania.

Shayo C.M. (2013). Report on Forests, Rangelands and Climate Change Adaptation in Tanzania

URT. (1995). National Land Policy (Sera ya Taifa ya Ardhi)

URT. (1999). National Land Act (Sheria ya Ardhi)

URT. (1999). Village Land Act (Sheria ya Ardhi ya Vijiji)

URT. (2007). Land Use Planning Act

URT. (2008). National Livestock Policy (Sera ya Taifa ya Mifugo)

URT. (2013). Land Use Planning Commission, Guidelines for Participatory Village Land Use Planning, Administration and Management in Tanzania – 2nd edition

URT (2013). National Agriculture Policy (Sera ya Taifa ya Kilimo)



Chapisho hili limetolewa kwa ufadhili wa kifedha kutoka Umoja wa Ulaya.
Mambo yaliyomo katika andiko hili ni jukumu la pekee la Henku, A., Swennenhuis, J., Mpanda, M. na si lazima yaakisi maoni ya Umoja wa Ulaya.
Usimamizi wa maeneo ya malisho: Wito wa kuwa na mtizamo mpana. GCCA Tanzania, andiko la kisera Na. 3. Dar es Salaam, Tanzania 2020



Barua pepe: delegation-tanzania@eeas.europa.eu
Tovuti: http://eeas.europa.eu/delegations/tanzania

https://facebook.com/EuropeanUnionTanzania
http://twitter.com/EUinTZ